

Maswali

1. Absalomu alikuwa nani?
2. Absalomu alitakaje ?
3. Watu walikuwa wafanye nini wakisikia sauti ya tarumbeta ?
4. Mjumbe alimwambia Daudi nini ?
5. Daudi alifanya nini?
6. Washauri wawili walimwambia Absalomu afanye nini?
7. Absalomu alipanda nini?
8. Ni nini ilifanyika kwa Absalomu mwituni ?
9. Nani aliwa Absalomu?
10. Daudi alifanya nini aliposikia Absalomu amekufa?

Majibu

1. Absalomu alikuwa mwana wa Daudi .
2. Absalomu alitaka awe mfalme.
3. Watu walisema, "Absalomu ni Mfalme."
4. Mjumbe alisema kwamba watu wote waisraeli wanampenda Absalomu.
5. Alitoroka
6. Mshauri wa kwanza alimwambia Daudi aende apigane papo hapo na wapili akamwambia aongoje mpaka watu wawe wamekuja wote.
7. Absalomu alipanda punda.
8. Nywele zake zilishikwa kwa mti .
9. Jemedari Yoabu ndiye alimuua Absalomu.
10. Daudi alilia

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

25 Daudi na Absalomu

Marejeo

2 Samweli 15—18

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu analinda wanaompenda lakini anawaadhibu waovu

Maneno maalum

1. Absalomu + Mwana wa Mfalme Daudi + ataka awe mfalme + anafanya watu wampende.
2. Daudi anasikia + Daudi anatoroka
3. Washauri + shauri + Daudi + Absalomu asiumizwe
4. Vita + punda + nywele + miti + Yoabu + Absalomu auawa + Absalomu azikwa
5. Daudi aambiwa + Daudi alia

25.1 Absalomu alikuwa mwana wa mfalme Daudi. Lakini alitaka kuwa mfalme badala ya baba yake Daudi. Absalomu aliambia watu kuwa atakuwa mfalme mzuri kuliko baba yake Daudi. Absalomu alituma wapelelezi kwa nchi ya Israeli yote. Akawafanya wakampenda. Wapelelezi waliambia watu, "Mkisikia sauti ya tarumbeta, mseme, Absalomu ndiye mfalme." Kwa hivyo wengi wakapenda Absalomu awe mfalme.

25.2 Mjumbe alienda kumwambia Daudi, "Watu wanapenda Absalomu na wanataka awe mfalme." Daudi alihuzunika na kuwaambia watumishi wake, "Lazima tutoroke la sivyo Absalomu atatuua."

Daudi na watumishi wake wakaondoka Yerusalem. Wakavuka mto na kwenda nyikani.

25.3 Absalomu na watu wote aliokuwa nao, wakaenda Yerusalem mpaka kwa ikulu ya mfalme.

Absalomu aliwaliza washauri wawili afanye nini. Mmoja alimwambia afuate Daudi na ampige kwa kuwa amechoka. Lakini mwingine aliyekuwa rafiki wa Daudi alimwambia aongeje mpaka watu wote wa Israeli wakusanyike pamoja ndipo aende apigane na Daudi.

Absalomu alifuata maneno ya mtu wa pili na akaongoja. Lakini Daudi akapumzika na kutayarisha jeshi lake kupigana. Aliwaambia askari wake wasimuumize Absalomu.

25.4 Askari wa Daudi walienda kupigana na jeshi la Absalomu ndani ya mwitu. Absalomu alipanda punda na alipokuwa akienda mbio chini ya miti, nywele yake ilijishika kwa matawi. Aliachwa akinginina kwa miti hali ameshikwa nywele.



Askari mmoja wa Daudi alimuona na akamwambia jemedari Yoabu. "Nilimuona Absalomu akinginina mtini."

"Kama ungemuuua ningekupea fedha nyingi sana." Askari alijibu, "Mfalme Daudi alisema tusimuue."

Lakini Yoabu alikimbia ndani ya miti mpaka akafika kwenye Absalomu alikuwa. Yoabu alikuwa na mikuki mitatu mkononi na akamchoma na zote wakati alikuwa hajakufa hapo mtini.

Yoabu alipiga tarumbeta na kuambia askari waache kupigana na watu wa Absalomu. Walichukuwa Absalomu na kumtupa ndani ya shimo kubwa na kuweka juu yake mawe mingi sana. Halafu wakakimbia na kurudi kambini.

25.5 Mtu mmoja alikimbia na kuenda kuambia Daudi aliekuwa akingojea. Daudi aliliza, "Absalomu ako mzima?" Huyo mtu akamwambia kwamba Absalomu amekufa.

Daudi alilia kwa sauti, "Ee Absalomu mwanangu! mwanangu." Ndipo Daudi akarudi Yerusalem na kuwa Mfalme tena. Alihuzunika sana juu ya Absalomu ingawaje alikuwa mtoto mbaya.



Jerusalem